# NADHARIA YA FASIHI SIMULIZI NA MAENDELEO KATIKA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

*Aldin K. Mutembei*

**1.0 Utangulizi**

Fasihi simulizi imekuwa ikifasiliwa kama fasihi inayohifadhiwa na kusambazwa kwa njia ya mdomo, ikitofautishwa na ile fasihi inayosambazwa kwa maandishi, yaani fasihi andishi. Mtu anapotafakari kwa kina fasili hii anaona kuwa ufafanuzi wa dhana ya fasihi simulizi haukuwa madhubuti kupambana na wakati unaosukumwa mbele kwa kasi na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Ufafanuzi wa fasihi simulizi wa Finnegan (1970) na ule uliotolewa takribani miongo mitatu baadaye na Wamitila (2003), umebaki kuwa ni ule ule. Hata pale ambapo baadhi ya wataalamu walithubutu kuvuka uzio wa wakati na kujaribu kuiangalia nadharia ya fasihi simulizi kama vile Okpewho (1992:3-5); Kezilahabi (1995: 59), au Wamitila (ameshatajwa uk.183), waliishia katika mzunguko ambao haukugusa uhusiano kati ya maendeleo ya sayansi na teknolojia na nadharia ya fasihi simulizi. Karibu wote wameshadidia umuhimu wa mdomo, sio tu katika kuumba, bali hata katika kuwasilisha na kuisambaza fasihi simulizi.

Kutokana na ukweli huo, mhakiki yeyote makini anakuwa na maswali mbalimbali yanayoibuliwa na mawazo hayo: Je mabadiliko katika namna ya usimulizi, uwasilishaji, na hasa usambazaji yanaweza kuiathiri nadharia ya fasihi simulizi? Je ni mambo gani mengine yanayopaswa kuangaliwa katika kuifafanua dhana ya fasihi simulizi? Na je kuna uhusiano gani kati ya nadharia ya fasihi simulizi na kukua kwa sayansi na teknolojia? Maswali haya ndiyo yaliyonisukuma kuandika makala haya kama kichokozi kuhusu nadharia ya fasihi simulizi.

Madhumuni ya makala haya ni kuiangalia dhana ya fasihi simulizi, na hasa fasihi simulizi ya Kiafrika kama inavyofafanuliwa na wataalamu mbalimbali wa fasihi. Katika kufanya hivi, lengo litakuwa kuonyesha udhaifu uliomo katika fafanuzi mbalimbali za fasihi simulizi zilizotolewa. Makala yanachukua mkabala wa kihistoria wa maendeleo ya jamii ya Watanzania kuhusiana na fasihi na teknolojia. Jamii hii ya Watanzania inachukuliwa kama kiwakilishi tu cha jamii za Waafrika popote walipo.

Makala haya yatakuwa changamoto katika kuingalia upya dhana ya fasihi simulizi. Yatakuwa kichocheo cha mjadala kuhusu nafasi ya fasihi simulizi katika maendeleo ya jamii. Yatawasaidia walimu na wanafunzi wa fasihi katika

sekondari na vyuo vya elimu ya juu kutetea umadhubuti wa nadharia ya fasihi simulizi.

## 2.0 Nadharia kwa ujumla

Wataalamu mbalimbali wameweka mawazo yao katika mpangilio na mtiririko wenye mantiki wakidhamiria kueleza ukweli fulani. Mawazo kama hayo huchukuliwa na watu wengine na kutumiwa katika miktadha mbalimbali, na kupata hitimisho linalotarajiwa au lenye kuhitilafiana. Mpangilio na mtiririko wa mawazo, wakati mwingine hutawaliwa na wakati. Mawazo fulani huwa kweli na kukubalika katika kipindi mahususi cha maisha na hupingwa au huonekana yana udhaifu katika kipindi kingine cha maisha. Kukubalika au kukataliwa kwake hutokana na sababu mbalimbali: wakati, eneo, ukweli katika uvumbuzi mpya, ufahamu, maendeleo katika nyanja za maisha na kadhalika. Katika makala haya tutachukua fasili ya nadharia kama ilivyofafanuliwa na (M. Bal, 1973:3) ambaye alisema:

> "Nadharia ni mpangilio wa mawazo ya jumla kuhusu sehemu mahususi ya ukweli fulani" (Tafsiri ya mwandishi)

Nguvu ya nadharia yoyote imo katika mpangilio wa mawazo. Kukubalika kwa nadharia yoyote kunatokana na namna mpangilio huo wa mawazo unavyoueleza ukweli fulani kama anavyoona huyo aliyepanga mawazo husika. Kwa kadri mpangilio huo unavyotumika katika sehemu mbalimbali, na kwa kadri unavyozidi kukubalika, ndivyo nguvu na ukweli wa nadharia hiyo unavyojidhihirisha, na hapa tunaongelea mpangilio wa mawazo kuhusu fasihi.

Kujidhihirisha kwa nadharia ya fasihi simulizi katika Afrika kulichochewa zaidi na Finnegan (*ameshatajwa*) ambaye aliandika kuhusu fasihi simulizi ya kiafrika. Ingawa, kama fasihi simulizi katika Afrika au penginepo ulimwenguni, imekuwapo kwa maelfu ya miaka na imeitangulia kwa mbali sana fasihi andishi (Mulokozi 1989:1), bado nadharia yake haijajitosheleza. Hata hivyo, Mulokozi (ameshatajwa) hatofautiani sana na mkabala tunaoujadili hapa anaposema:

> "kwa upande wa muktadha na namna ya uwasilishaji, tunazingatia *ukweli wa msingi kuwa fasihi simulizi ni sanaa inayopita, isiyofungiwa katika umbo_maalumu,* wala matini maalumu, *yasiyobadilika...*" (Mulokozi, 1989:2) (msisitizo wa mwandishi).

Kama tutakavyoonyesha kumekuwa na udhaifu katika kufikiria dhana za msingi katika nadharia ya fasihi simulizi. Mambo haya yamesababisha kuyumba kwa maana ya fasihi simulizi na kutofafanuliwa kwa dhima yake katika maisha kama inavyotarajiwa. Hoja yangu ni kwamba, dhana ya fasihi

simulizi, pamoja na istilahi nyingine zinazoambatana na ufafanuzi wa fasihi simulizi hazina budi kuangaliwa upya.

**3.0 Fasihi Simulizi inavyofafanuliwa**

Kwa muda mrefu wanafunzi na walimu wao wa sekondari na hata vyuo vya elimu ya juu wamekuwa wakiifafanua fasihi simulizi kwa namna moja au inayokaribiana. Tokea ilipofafanuliwa na Finnegan (ameshatajwa) zaidi ya miongo mitatu iliyopita hadi leo, kimsingi ufafanuzi umebaki kuwa uleule. (Taz.) Wamitila (ameshatajwa) Katika kipindi hicho chote wanataaluma kama Balisidya (1979), Mbunda (1992), Mulokozi (ameshatajwa), Bukenya na wengineo (1997) wameshikilia nadharia ya fasihi simulizi kama kwamba fasihi imetuama, yaani imebakia vilevile bila kubadilika. Kutuama huku ambako katika makala haya tunakuangalia kama udhaifu, kumetokana na sababu kadhaa. Mojawapo ni kwamba katika kuifafanua dhana ya fasihi simulizi maana za namna inavyotolewa na kuhifadhiwa zimewekwa pamoja na kile kitolewacho. Suala linalotawala dhana ya fasihi hii ni njia ya uwasilishwaji ambayo ni mdomo. Kwa maneno mengine, "chombo" kinachoiumba na kuiwasilisha fasihi simulizi kimeonekana kuwa ni muhimu sana kuwa katika maana ya dhana nzima ya kazi inayowakilishwa. Kama kwamba bila hicho, basi hakuna fasihi simulizi. Tuone baadhi ya mifano ya hoja hii:

Mkabala wa Finnegan (ameshatajwa uk. 2) kuhusu fasihi simulizi unaelezwa ifuatavyo:

> "Fasihi simulizi yaweza kuelezwa kwamba, hutegemea msanii ambaye huiumba kwa maneno katika tukio maalumu .... hapana njia nyingine ambayo inaweza kutambuliwa kama zao la fasihi... bila ya kutambuliwa kwa njia ya mdomo na kutolewa moja kwa moja toka kwa mwimbaji au mzungumzaji, sio rahisi kwa fasihi hii isiyoandikwa kuendelea kuwapo..." (tafsiri ya mwandishi).

Hapa Finnegan anatueleza mambo mawili ambayo kwake anayaona ni ya lazima ili fasihi simulizi iwepo: kwanza ni mwanafasihi mwenyewe ambaye huwa ana kwa ana na hadhira isikilizayo fasihi itolewayo, na pili, ni njia ya utolewaji ambayo ni mdomo.

Suala hili kama nitakavyoonyesha baadaye halifikirii kabisa mabadiliko ambayo yanaletwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Kwa mfano ana maana gani anaposema:

> "...hapana njia nyingine ambayo inaweza kutambuliwa kama zao la fasihi simulizi... bila ya kutambuliwa kwa njia ya mdomo na kutolewa moja kwa moja toka kwa mwimbaji...." Finnegan (ameshatajwa uk. 2). (Tafsiri ya mwandishi)

Je leo tunaposikia hadithi zikisimuliwa katika televisheni, na kisha tukaona na kusikia sauti nyingine kama vile za simba, radi au zimwi ambazo ni za kujifaragua ambazo zimetengenezwa na fundi mitambo au na mwongozaji kipindi ili kuleta athari fulani, hii athari itaelezwa vipi? Wakati mwingine inawezekana kuwa yule msimulizi mwenyewe havifahamu vipengele hivyo. Ni tafsiri tu ya mwongoza kipindi au fundi mitambo. Njia hii ya televisheni ambapo msimulizi hayupo ana kwa ana na hadhira, ina mguso pengine zaidi kuliko msimulizi ambaye hana vyombo, ni mdomo tu. Kwa hiyo, suala la umuhimu wa mdomo pekee halina budi kuangaliwa upya.

Akizidi kufafanua suala la umuhimu wa mdomo mwanafasihi mwingine (Balisidya 1980:1) anasema:

> "Fasihi simulizi ni ile aina ya fasihi ambayo hutegemea sana usanii wenye sauti, mtawanyiko na usambazwaji wake. Hata kama inaweza kutunzwa kwa maandishi, na kwa kweli maandishi yanaweza kusaidia kuongeza utunzi, fasihi simulizi hubaki ni ya mdomo. Kama mawasiliano yoyote ya maneno, fasihi simulizi hutumia sikio na jicho"

Mahali pengine Matteru (1983: 26) anaongezea vipengele vingine ili kuikamilisha hoja yake kuhusu dhana ya fasihi simulizi anaposema:

> "Fasihi simulizi ni aina ya fasihi ambayo hutumia mdomo katika kuumbwa, kuwasilishwa na kusambazwa kwa wasikilizaji na watumiaji wake... hutegemea sana nyenzo mbalimbali za kuonekana na kusikika zitumiwazo na binadamu katika kujieleza. Mathalani fasihi simulizi hutegemea utendaji ili kukamilika: msogeo, vitabia, miondoko n.k ni vipengele muhimu sana..."

Hapa Matteru anausogeza mjadala hatua moja zaidi. Anaongelea 'aina' ya fasihi kwa maana kwamba anapenda kuitofautisha fasihi moja kutoka nyingine. Pili anaongelea sio kutolewa tu, bali pia kuumbwa yaani 'utengenezaji' na usambazaji. Kwa kuwa Matteru ametuingiza katika kufafanua aina moja ya fasihi, hatuna budi kuangalia aina nyingine ya fasihi ambayo hakuitaja kwa kirefu, tuone inafafanuliwaje ili tuweze kuipambanua miongoni mwa sanaa nyinginezo. Finnegan (ameshatajwa) analinganisha fasihi hizi mbili, na kuelezea uhusiano wa *uumbwaji* wa fasihi na *usambazwaji* wake kwa kusema:

> "Kwa upande wa fasihi andishi, kazi ya fasihi inaweza kusemwa kuwa ipo, inajitosheleza na kujitegemea katika nakala moja ya kitabu, hivi kwamba maswali kuhusu tuseme, muundo, nakala, na machapisho ya nakala nyingine yanaweza kuonekena kuwa ni mambo ya ziada ingawa hatuyatupi moja kwa moja kuwa hayana maana. Yaani, kuna tofauti kati ya uumbwaji wa fasihi andishi na usambazwaji wake." (Finnegan, 1970:2)

Kama Matteru, Finnegan anaelekea kuona kuwa dhana na usambazwaji wa fasihi simulizi ni mambo yanayotegemeana, tofauti na fasihi andishi ambapo kila kimoja hujitegemea.

Ingawa hizi ni tofauti ndogo, lakini suala kubwa limo katika utolewaji wa fasihi simulizi na hasa katika kipengele cha mdomo. Hata wale walioangalia maana ya fasihi kwa ujumla, wametofautisha fasihi simulizi kutoka katika dhana ya jumla ya fasihi kwa kuzingatia kipengele cha mdomo. Balisidya (1979) alifafanua hivi katika kipengele hiki:

> "Fasihi simulizi ni fasihi inayotegemea mdomo katika kutolewa na kuenezwa kwake…" (Balisidya, 1979).

Kutegemea mdomo maana yake ni kuwa pasipo mdomo, kuwepo kwa fasihi simulizi kunakuwa hakujakamilika. Mwingine aliyetilia mkazo kipengele hiki ni Okpewho aliposema:

> "Fasihi hutumika zaidi kwa maana maalumu kumaanisha matini bunifu ambayo hugusa hisi na fikra zetu…Fasihi simulizi humaanisha 'fasihi itolewayo kwa neno la mdomo"… (Okpewho, 1992: 3).(Tafsiri ya mwandishi)

Mulokozi naye ana mtazamo kama wa Matteru na Okpewho anaposema:

> "…fasihi simulizi ni fasihi inayotungwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya mdomo na vitendo bila kutumia maandishi." (Mulokozi, 1996: 24).

Maelezo ya Matteru, Okpewho na Mulokozi hapo juu hayatofautiani sana na ya akina Bukenya na wenzake wanapotoa ufafanuzi ufuatao:

> "Watu wengi wanajua kwamba, neno "fasihi simulizi" linamaanisha hadithi za jadi, nyimbo, mashairi, vitendawili na methali ambavyo hutolewa kwa neno la mdomo. Watu husimulia hadithi, hutongoa mashairi na kuimba nyimbo. Tena hubadilishana vitendawili, utani, mafumbo na methali. Twayaita haya "simulizi" maana huwasilishwa kupitia katika tamko. Twayaita "fasihi" kwakuwa yanatumia lugha kibunifu…" (Bukenya, Gachanja, na Nandwa, 1997: 3) (tafsiri ya mwandishi)

Mbali na kuifafanua fasihi simulizi kwa kuzingatia utolewaji, wanataaluma wengine kama vile Mbunda (1992) na Wamitila (ameshatajwa) wanaingiza dhana mpya ya namna ya *kuihifadhi* fasihi hii. Yaani dhana ya fasihi simulizi haiangaliwi tu katika namna ya utolewaji bali pia katika namna

inavyohifadhiwa. Hata hivyo, wanataaluma hawa wanatofautiana kwa kipengele kimoja cha msingi: Mmoja anasema fasihi hii inahifadhiwa kwa *kichwa* na mwingine inahifadhiwa kwa *mdomo*. Mbunda anasema:

> "Kama ilivyo fasihi andishi, fasihi simulizi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha. Kazi hii ya sanaa *huhifadhiwa* kwa kichwa na kusambazwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo…" (Mbunda, 1992: 7) (Msisitizo ni wa mwandishi).

Wakati Mbunda anazungumzia fasihi simulizi huhifadhiwa kwa kichwa na kusambazwa kwa mdomo, Wamitila anasema inahifadhiwa kwa mdomo:

> "Sanaa hii iitwayo fasihi inaweza *kuhifadhiwa kwa njia mbili kuu: kwa njia ya mdomo na kimaandishi.* Aina ya kwanza, ambayo tunajihusisha nayo katika sehemu ya kwanza inajulikana kama fasihi simulizi…" ( Wamitila, 2003: 13.) (Msisitizo ni wa mwandishi).

Na kisha anaendelea:

> "… katika 'tamaduni andishi', ambazo zimeathiriwa na mfumo wa kimaandishi, hiyo inayojulikana kama fasihi simulizi sio simulizi tena bali inahifadhiwa kwa njia mbalimbali kama kwa vinasa sauti, kanda za video na kompyuta…" (Wamitila, ameshatajwa, uk.13-14).

Mtazamo wa Wamitila unatofautina na wa wenzake ambao wamekuwa wakivichukulia vipengele vya: *kuumbwa, kuhifadhiwa na kusambazwa* kwa fasihi simulizi kuwa ni vipengele ambavyo havitenganishwi kutoka dhana ya fasihi simulizi. Lakini, kwa kusema hivi, Wamitila (ameshatajwa) anaonyesha kuwa maana ya fasihi simulizi na namna inavyosambazwa ni mambo ambayo hayana budi kutenganishwa. Aidha, Wamitila (ameshatajwa) anaelekea kusema kuwa dhana ya fasihi simulizi ni tofauti kwa wale wenye utamaduni wa maandishi, na wale wasiokuwa na utamaduni huo. Kwa sababu hizi, baadhi ya dhana ambazo zimekuwa zikitolewa kwa kuambatanishwa na maana ya fasihi simulizi hazina budi kuangaliwa upya.

**4.0 Mjadala**

Kwa ujumla, uhakiki wa dhana ya fasihi simulizi haujawa makini na madhubuti. Kumekuwa na utata katika vipengele ambavyo kimsingi ni tofauti. Makala haya yanaegemeza mjadala wake katika jedwali lifuatalo:

| | Kutolewa/ Kuwasilishwa | Kuhifadhiwa | Kusambazwa | Umbo maalumu | Matini yake |
|---|---|---|---|---|---|
| Kale | Mdomo. Msanii yupo ana kwa ana na hadhira, akifa na njia hii ya mdomo inakwisha. | Kichwani mwa msanii | Msanii mwenyewe kupitia mdomo wake | Hakuna umbo maalumu, ni huru | Inabadilika badilika |
| Sasa | ? | ? | ? | ? | ? |

*Jedwali Na. 1: Mtazamo wa kale kuhusu vipengele vya fasihi simulizi*

Vipengele hivi, vinaelezwa kama vinafanana mahali fulani, na mahali pengine vimetofautishwa. Isitoshe, wataalamu mbalimbali wamekuwa na dhana tofauti ya fasihi simulizi kama tulivyoona hapo juu. Tuangalie vipengele vichache vinavyoleta utata katika kuifafanua dhana ya fasihi simulizi.

### 4.1 Kuwasilishwa

Suala la uwasilishwaji wa fasihi simulizi bado linaleta utata, maana kwa walio wengi wanaposema kuwa fasihi simulizi inawasilishwa kwa mdomo, wanamaanisha kuwa inatolewa toka katika mdomo wa msanii ambaye anakuwa ana kwa ana na hadhira inayomsikiliza. Kuhusiana na suala hili, Wamitila (ameshatajwa) anasema hivi:

> "Kimsingi, fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya mdomo kwa kusimuliwa, kuimbwa, kutongolewa au kughaniwa…" (Wamitila, 2003: 14).

Kwa kusema hivi mwandishi huyu amechanganya dhana za kuhifadhiwa na kuwasilishwa, kama tulivyoeleza hapo juu.

Aidha anaendelea kuweka vipengele vingine vinavyoambatana na uwasilishaji kwa kusema:

> "Uwasilishwaji wa fasihi simulizi pamoja na ufanisi wa uwasilishaji huo *hutegemea* 'viambato' vingine kama mavazi, mabadiliko ya kihisia ya mtambaji, miondoko…" (Wamitila, 2003:15). (msisitizo ni wa mwandishi).

Hapa mwandishi anamaanisha kuwa msanii huwapo palepale na akaonekana.

Kwa kutumia neno "kutegemea" Wamitila (ameshatajwa) anaonyesha kutokukamilika kwa dhana ya fasihi simulizi bila ya msaada wa viambato hivyo. Swali la msingi hapa ni je kama msimulizi haonekani uwasilishaji wa fasihi simulizi unaathirika au la? Jambo hili litaangaliwa tena tutakapozungumzia fasihi simulizi katika vyombo vya habari vinavyotoa sauti kama redio na televisheni na hata wakati huu, intaneti (wavuti).

## 4.2 Wakati

Pale mwanzoni tuliona kuwa Finnegan (ameshatajwa) anaongelea utolewaji wa fasihi simulizi unaoambatana na wakati. Wamitila (ameshatajwa) pia anaonyesha kuwa ubunifu wa fasihi simulizi huhusishwa na wakati huohuo wa kutolewa kwake. Anasema:

> "Mtambaji anaweza kuingiza sifa za ubunifu wakati wa kuitamba au kuisimulia hadithi yake..." (Wamitila, 2003:14).

Jambo hili la wakati limeongelewa na wengine kama vile Mbunda, Balisidya na Okpewho (wameshatajwa). Mulokozi (ameshatajwa uk. 25) kwa mfano, anasema:

> "...lakini matini na mbinu za kisanii hutungwa papo kwa papo wakati wa uwasilishaji. Hivyo tungo hizo hazikaririwi kama baadhi ya watu wanavyofikiri...".

Kwa kusema hivi wataalamu hao wanaonyesha kuwa ukamilifu wa fasihi simulizi huendana na sifa zake za kuwapo kwa ubunifu wa papo kwa papo au mbinu ya kujifaragua. Swali linalozua utata katika kipengele hiki ni, je katika redio au televisheni, simulizi zitolewazo, zitaitwa fasihi simulizi? Kama ndivyo, mbona zinakiuka kipengele hiki cha ubunifu wa wakati huo huo? Kwa maneno mengine, je ikiwa mtu ameandaa kipindi chake na kukirusha hewani siku apendayo kitakuwa na sifa hii? Kama usimuliaji huo hautakuwa fasihi simulizi kutokana na kukosa sifa hizo, je utaitwa nini? Kwa hakika simulizi za redioni, kwenye televisheni au intaneti, ni fasihi simulizi. Hazina sifa hii ya kale, lakini ni fasihi simulizi na hivyo zinatoa changamoto. Dhana ya fasihi simulizi inabidi iangaliwe upya.

## 4.3 Wakati maalumu

Mbali na ubunifu unaoendana na wakati, wataalamu wengi wanaonyesha kuwa fasihi simulizi hutolewa kwa wakati maalumu. Wamitila (ameshatajwa) anasema hivi:

> "...kuna vipindi maalumu vya kutega vitendawili na vingine vya kusimuliana hadithi. Katika jamii nyingi, usimulizi au utambaji wa hadithi hautokei kila wakati bali kwa wakati maalumu hasa jioni" (Wamitila, 2003: 15).

Halikadhalika Mulokozi (ameshatajwa uk. 25) ana mtazamo huo huo kama asemavyo:

"...wakati ni muda maalumu kihistoria, au majira maalumu ya utendaji huo."

Suala la wakati maalumu lilitokana na kazi katika jamii. Kwa mfano katika jamii nyingi za wakulima, asubuhi na mchana ni kipindi watu wanapokuwa kazini, jioni wanarudi majumbani mwao na wakiwa katika kazi za nyumbani wakisubiri mlo ndipo tanzu nyingi za fasihi simulizi zilipotolewa. Jambo hili pia liliendana na kiwango cha maendeleo ya sayansi na teknolojia kuhusiana na vifaa vya upishi. Maendeleo ya siku hizi yanaruhusu watu kupika kwa majiko ya umeme, gesi, mkaa na tena wapishi sio lazima wawe mama wa nyumba. Swali linaloleta utata hapa ni je katika redio au televisheni ambapo hakuna wakati huo maalumu simulizi zitolewazo zitafaa kuitwa fasihi simulizi? Kama nilivyosema awali, simulizi hizo pia ni fasihi simulizi hata kama kipengele hiki cha wakati hakiendani na simulizi hizo.

**4.4 Hadhira**

Suala la hadhira "hai" limeongelewa kwa kina na baadhi ya wataalamu. Mulokozi (ameshatajwa uk. 24- 25) anaifafanua fasihi simulizi kwa kusema:

> "...hivyo fasihi simulizi ni tukio linalofungamana na muktadha (mazingira) fulani wa kijamii, na kutawaliwa na mwingiliano wa mambo sita: fanani, hadhira, fani inayotendwa, tukio, mahali, na wakati".

Katika kipengele cha hadhira anasisitiza kuwa:

> "... ni wasikilizaji, ambao mara nyingi pia huwa ni washiriki ... na wahakiki ...wa sanaa hiyo inayowasilishwa na fanani".

Hapa Mulokozi anaonyesha kuwa hadhira katika fasihi simulizi huwa "hai", yaani inayoshiriki katika kuiboresha fasihi hiyo; hadhira inayosikiliza na kutenda.

Jambo hili amelizungumzia pia Wamitila (ameshatajwa uk.15) anaposema:

> "... Hadhira ya fasihi simulizi inaweza kuwa tendi, ambayo inashiriki na kuchangia katika uwasilishwaji wa kazi inayohusika.".

Wamitila anaonyesha kuwezekana na kutokuwezekana kwa ushiriki wa hadhira katika uwasilishwaji wa fasihi simulizi.

Suala lenye kutatiza hapa ni, je ikiwa masimulizi katika redio au kwenye televisheni yatakubalika kuwa ni fasihi simulizi hadhira yake itakaaje? Je ni tuli,

tendi, au changamano? Jambo hili la ushiriki wa hadhira, litakalojadiliwa baadaye kidogo, lina uhusiano na msanii au msimulizi wa fasihi simulizi na uhuru alionao.

### 4.5 Uhuru wa msanii

Kutokana na suala la hadhira lililojadiliwa katka kipengele cha 4.4 hapo juu wataalamu wengi wanaona kuwa msanii wa fasihi simulizi ana uhuru wa pekee ambao yule wa fasihi andishi hana. Mulokozi (ameshatajwa uk. 25) anasema hivi:

> "... lakini matini na mbinu za kisanii hutungwa papo kwa papo wakati wa uwasilishaji. Hivyo tungo hizo hazikaririwi kama baadhi ya watu wanavyofikiri...".

Hii ina maana kuwa mtungaji anao uhuru kutokana na mazingira ya uwasilishaji. Kwa kuifafanua hoja hii Wamitila (ameshatajwa uk. 16) anasema:

> "mtambaji au mwasilishaji wa fasihi simulizi ana uhuru mpana sana wa kuweza kubadilisha mbinu na hata muundo wa kazi anayoiwasilisha papo kwa papo..."

Je uhuru huu upo pia katika simulizi za redioni? Kama haupo, simulizi hizo zinapunguziwa sifa ya kuwa fasihi simulizi kwa sababu hiyo? Suala la uhuru wa msanii linaendana sana na lile la uthabiti na hata uhifadhi wa fasihi simulizi tunapoangalia kuwepo kwa fasihi hii katika vyombo vya kisasa vya habari na video.

### 4.6 Uhifadhi na hali ya uthabiti

Kwa kutofikiria hali ya kuwepo kwa fasihi simulizi katika vyombo vya habari kama vile redio au televisheni, au hata katika video, wataalamu wengi wamejadili suala la uhifadhi wa fasihi simulizi, na uthabiti wake kama jambo ambalo ni gumu kufikirika. Mulokozi (ameshatajwa uk. 28) anasisitiza kuwa fasihi hii inahifadhika kwa njia ya mapokeo, akimaanisha kuwa inahifadhiwa vichwani mwa watu. Akifafanua ugumu wa fasihi simulizi kutokuwa thabiti Mulokozi anasema:

> "Hubadilika haraka kutegemea mahitaji ya hadhira na wakati. Ni nadra kudumu katika hali ile ile baada ya mtunzi kufariki".

Akiunga mkono suala hili Wamitila (ameshatajwa uk. 16) ana maoni yafuatayo:

> "Kuhifadhiwa kwa fasihi simulizi kuna ugumu mkubwa kukilinganishwa na kwa fasihi andishi. Hii ni fasihi ya kupokezana kwa njia ya mdomo. Katika

kupokezanwa huku sehemu fulani inaweza kupotea au kusahaulika kwa sababu nguzo kuu ya kuhifadhi ni uwezo wa mtu kukumbuka… "

Mawazo haya yamejengeka katika msingi kwamba kwa vyovyote vile viwavyo, fasihi simulizi ni sanaa iliyo kichwani mwa mtu, inayosambazwa kwa mdomo wa aliyenayo au anayeisikia. Suala hili kama vile tulivyoona yale mengine halitilii maanani kuwepo kwa fasihi simulizi katika vyombo vya kisasa vya kunasia sauti na hata pengine picha, yaani redio, televisheni, video na mawasiliano mengine kama ya intaneti.

Hata hivyo, ijulikane kuwa tunapoipata fasihi simulizi kutoka katika vyombo hivi vya kisasa, hali ya uthabiti wa fasihi simulizi inakuwa ni imara kabisa sawasawa na uthabiti uliopo katika fasihi andishi. Kwa jinsi hiyo, tunajenga hoja kwamba dhana ya fasihi simulizi na vipengele vyake haina budi kuangaliwa upya ikizingatia muktadha wa maendeleo ya sayansi na teknolojia jambo ambalo sasa tutalijadili kwa kina hapo chini.

## 5.0 Hali ya fasihi simulizi kwa kuzingatia maendeleo ya sayansi na teknolojia

Kwa kuzingatia maendeleo yanayoletwa na sayansi na teknolojia siku hizi imeonekana kuwa dhana ya fasihi simulizi ya kale ina upungufu. Katika jedwali la kwanza (Na. 1) tumeonyesha mawazo yanayotolewa na baadhi ya wataalamu wa fasihi simulizi. Katika sehemu ya pili inayoonyesha wakati wa sasa tumeacha alama za kuuliza ili kuacha maswali katika mjadala. Hebu tuangalie jedwali lifuatalo ili tufanye ulinganifu:

| | **Kutolewa/ Kuwasilishwa** | **Kuhifadhiwa** | **Kusambazwa** | **Umbo maalumu** | **Matini yake** |
|---|---|---|---|---|---|
| *Sasa* Sayansi na Teknolojia | a) Mdomo.<br>b) Chombo kama redio, tv, video, kanda<br>c) Sio lazima msanii awepo. | Chombo kama redio, tv, video, intaneti | Sauti ya msanii inapitia katika vyombo | Linaweza kuwa maalumu lisilobadilika<br>.<br>Sio lazima kuwa huru | Inaweza kutobadilika hasa ikihifadhiwa katika vyombo. |
| *Kale* | a) Mdomo.<br>b) Msanii yupo ana kwa ana na hadhira.<br>-Akifa na njia hii ya mdomo inakwisha. | Kichwani mwa msanii.<br>Akifa fasihi hii inatoweka | Msanii mwenyewe kupitia mdomo wake | Hakuna umbo maalumu, ni huru | Inabadilika badilika |

*Jedwali Na. 2: Mtazamo wa sasa kuhusu vipengele vya fasihi simulizi*

Hali ya fasihi simulizi katika muktadha wa sayansi na teknolojia haina budi iangaliwe sambamba na maendeleo ya binadamu ambaye fasihi hiyo ni mali yake. Mtazamo huu umeelezwa vizuri zaidi katika dondoo lifuatalo:

> "usiione teknolojia kama kitu huria ambacho kinategemea tu matumizi. Teknolojia ndiyo inayokata shauri juu ya mwelekeo wa kibinadamu ingawaje tunaigundua wenyewe..." (Kezilahabi, 1995: 59).

Ugunduzi katika sayansi na teknolojia huwa na manufaa kwa binadamu kwani humsaidia katika kurahisisha utendaji wa kazi hata katika kuwasilisha au kuhifadhi fasihi simulizi. Watoto waliozaliwa katika zama hizi za sayansi na teknolojia wengi wao wanakulia katika ulimwengu ambao unawanyima muda wa kukaa na wakubwa zao (wawe wazazi, mababu/mabibi, au kaka/dada zao) ili kusimuliwa hadithi, kughaniwa, kuimbiwa n.k ingawa labda sehemu za vijijini bado watoto wengine wanapata fursa kama hiyo. Walio wengi hasa wale wa mijini, hawapati fursa ya kuifaidi fasihi simulizi katika dhana na umbo la kale, lile linalosisitiza kusambazwa kwa njia ya mdomo, na kuhifadhiwa kichwani. Hata hivyo, kwa dunia inayobadilika, watoto hao, wawe wale walioko majumbani, shuleni au ambao wamemaliza kiwango fulani cha elimu, wanaipata fasihi simulizi katika maana na umbo linaloendana na sayansi na teknolojia ya wakati wao.

Kama dunia ibadilikavyo kwa upande wa sayansi na teknolojia, ndivyo fani na tanzu zake za kisanaa zinavyobadilika au zinavyopaswa kubadilika. Na hapa tunakubaliana na Kezilahabi (ameshatajwa uk. 59) kama anavyosema:

> "'...ieleweke kwamba fasihi ya Kiswahili imo katika karne ya teknolojia, lazima ijieleze katika mazingira hayo na kukua kwake hakuwezi kutenganishwa na teknolojia ya neno...Tusiione teknolojia kama kitu huria ambacho kinategemea tu matumizi. Teknolojia ndiyo inayokata shauri juu ya mwelekeo wa kibinadamu ingawaje tunaigundua wenyewe."

Fasihi ya Kiswahili kama fasihi nyingine yoyote, inajichomoza kutoka katika jamii ambayo inaandamwa na mabadiliko ya aina mbalimbali. Hali kadhalika, fasihi simulizi inaandamwa na mabadiliko hayo. Kwa hivyo ni muhali kwa fasihi simulizi kung'ang'ania dhana ileile ya fasihi simulizi iliyotolewa zama za zana za mawe, katika zama hizi za sayansi na teknolojia. Kutokubadilika na kwenda na wakati ni kutoitendea haki taaluma. Baadhi ya vipengele vifuatavyo tunavipa mwelekeo mpya unaolenga kuamsha changamoto ya mjadala utakaoweka uthabiti wa nadharia mpya ya fasihi simulizi.

### 6.0 Chombo cha kuwasilishia fasihi simulizi

Tumekwishaona kwamba, mdomo umetumiwa na wataalamu wengine kuzungumzia namna fasihi simulizi inavyosambazwa kutoka kizazi kimoja

kwenda kingine. Ama hapa tunaweza kuuona mdomo kama chombo tu cha kutolea au kuwasilishia fasihi hiyo.

Swali tunaloweza kujiuliza hapa ni, je tunaposikiliza redio (au televisheni), ni "chombo" gani kinachotusambazia fasihi hiyo? Ni redio yenyewe au stesheni ya redio? Je ni mdomo wa yule msimuliaji au mtangazaji wa redio? Na kama ni kwa njia ya intaneti (au wavuti) je ni nani hasa ambaye anatusambazia fasihi hiyo? Maana kama ilivyo kwenye televisheni, kwenye intaneti pia waweza kuona matendo na hata kusikia sauti, ingawa mahali pengi kuna kompyuta ambazo hazijaunganishwa kutoa sauti lakini jambo hili lipo na linawezekana. Hapa hatuna budi kujiuliza swali la msingi katika ujenzi wa nadharia yetu: *Kuwasilisha ni nini*? (maana kuna watu wawili: mmoja anatumia *kalamu* anaandika mawazo yake. Mwingine anatumia *mdomo* anatuambia mawazo yake. Anayetumia kalamu, tunayaona *maandishi*, na anayetumia mdomo tunaisikia *sauti*, matokeo ni maandishi na sauti. Hivyo, kuutaja mdomo kungelikwenda sambamba na kuitaja kalamu; vyombo vya kuwasilishia fasihi. Lakini kuna tofauti kubwa wataalamu wanapoongelea fasihi andishi.

Katika fasihi andishi, wataalamu wanaongelea *matokeo* - maandishi. Kwa nini katika fasihi simulizi wataalamu hawayaongelei *matokeo* - *sauti*, bali huongelea "kifaa kinachotumika kutolea sauti". - mdomo? Inawezekana thamani na nguvu iliyowekwa katika maandishi kutoka katika tamaduni zenye uandishi ndilo jambo linalotutatiza. Bado wataalamu wengi wamefanywa kutothamini na kutotambua nguvu na thamani ya sauti. Wanaona ni kitu cha kupita, sio kitu thabiti n.k. Hizi ni hoja zisizozingatia suala la muda na maendeleo katika jamii, zilizopandikizwa na wale wanaoona fahari kuzungumzia maandishi na nguvu yake.

**7.0 Hadhira katika muktadha wa sayansi na teknolojia**

Ikumbukwe kwamba hapo awali hadhira ilikuwa inaangaliwa kama watu watakaokuwa na msanii aitoaye fasihi simulizi ana kwa ana. Katika hali hiyo ikaongelewa hadhira inayochangia uhai wa fasihi hiyo, na hata kuathiri uumbwaji wake, ikaitwa hadhira tendi. Hata hivyo dhana ya hadhira haina budi iwekwe katika mapana yake.

Katika muktadha wa maendeleo ya sayansi na teknolojia, hadhira ni changamano. Sio lazima iwepo ana kwa ana na msimuliaji. Na wala sio lazima iathiri usimuliaji. Hadhira ina sura mbalimbali kama zifuatazo:

*7.1 Hadhira yenye athari.*

Hii ni hadhira ambayo huwapo ana kwa ana pamoja na msanii wa fasihi simulizi. Hii ni ya kawaida ambayo wengi tumeizoea. Ni ile ambayo huzunguka

moto ikimsikiliza msanii akisimulia. Huweza kupiga makofi, kushangilia, kucheka, kuguna au kulia na hivyo kuleta athari katika usimulizi.

*7.2 Hadhira isiyo athari*

Hii ni ile hadhira inayozunguka redio au televisheni huku ikiwa haina mawasiliano na msanii aliye ndani ya redio, televisheni au mkanda wa video. Inaweza ikashangilia, ikazomea, ikasikitika n.k, lakini yote hayo, msimuliaji hatakuwa na habari nayo. Na kwahiyo, haina athari katika usimulizi.

*7.3 Hadhira ya nusu-athari, na nusu iso athari*

Hii ni hadhira ambayo ama inaonana na msanii ana kwa ana ama hawaonani. Hadhira inayonana ana kwa ana na msanii ni kama vile wakati vipindi vya masimulizi hutolewa studio mbele ya wasikilizaji kadha ambao wamo kwenye studio pamoja na msimuliaji. Wanaonana naye ana kwa ana. Hawa huwa ni ama watoto, au watu wazima kutegemea na masimulizi yatolewayo na redio au televisheni fulani. Hao watakaokuwa studio ni hadhira ambayo itarekodiwa pamoja na msimulizi wao. Wataweza kuwa na athari kwa msimuliaji ambaye wanaye studioni ana kwa ana wakati ule. Wakisharekodiwa, kipindi chao kinarushwa hewani na kusikilizwa na watu wengine ambao hawamo studio. Hii ndiyo hadhira isiyoonana ana kwa ana na msanii. Katika mazingira haya kuna hadhira mbili ambazo zinasikiliza usimulizi ule ule. Moja ni ile inayoweza kuathiri usimulizi, kwakuwa imo studio (watu wachache) na nyingine ni ile iliyo nje ya studio ambayo haina uwezo wa kuathiri masimulizi. Hii ya nje inaweza kubadilika ipendavyo, lakini ile ya ndani hubaki kuwa ileile wakati kipindi kinapokuwa kimesharekodiwa. Hadhira zote mbili (moja ya wasikilizaji, na nyingine ya wasikilizaji washiriki) haziwezi kuwasiliana. Kwa hiyo kwa msimuliaji baadhi ya wanahadhira wake wanaweza kuathiri usimulizi na baadhi hawawezi.

Tena kuna aina nyingine ya hadhira tunapojadili suala la studio. Hii ni hadhira ile ambayo, japo iko nje ya studio, inamsikia msimuliaji, na inaweza kuwasiliana naye kwa kupiga simu tokea popote ilipo kwenda studio, baada ya msimuliaji kumaliza masimulizi yake au katikati ya usimuliaji kwa kadri kipindi kitakavyokuwa kinaruhusu. Sura hizi zote zinaifanya dhima ya hadhira ibadilike kutoka katika dhana ya kimapokeo kwenda katika dhana ya kisasa. Mabadiliko hayo hayana budi kuangaliwa pia katika vipengele vya wakati na nafasi fasihi simulizi inapotolewa.

**8. 0 Wakati na Mahali katika muktadha wa sayansi na teknolojia**

Kimapokeo fasihi simulizi ilifanyika saa za jioni, kando ya moto au barazani. Suala hili linatudokeza sio tu maendeleo ya jamii husika katika ujenzi wa

nyumba (barazani na mahali pa kuotea moto), lakini pia linatuonyesha hali ya amani na usalama (watu kukaa na kusimuliana hadithi).

Nyumba nyingi za vijijini na mazingira ya kupika bado zina nafasi ya utolewaji kama huo wa kimapokeo wa fasihi simulizi. Lakini wakati wa mabadiliko unakuja kwa haraka, hasa mijini. Ujenzi wa nyumba nyingi hauruhusu mahali pa kuotea moto, kwani wengi hawatumii mafiga, bali majiko ya mkaa, ya mafuta ya taa, ya gesi au yale ya umeme. Kwa namna hizi za upishi suala la kuuzunguka moto na kusimuliana hadithi linabaki katika historia tu.

Aidha, kwa vile fasihi simulizi hutolewa redioni, inaweza kusimuliwa wakati wowote na mahali popote ambapo kipindi hicho kinasikika kwa saa na wakati huo. Kwa mfano, masimulizi ya hadithi za redioni kwa darasa la nne na la tano katika shule za msingi, hufanyika kati ya saa 4 na saa 5 asubuhi kwa siku za Jumatano katika redio Tanzania. Kama darasa husika halina nafasi mwalimu anaweza kukirekodi kipindi hicho na kuwafungulia wanafunzi ili wakisikie wakati wanapokuwa na nafasi.

Majumbani mijini, watoto hawazunguki moto tena, bali husubiri wakati kipindi kinaporushwa hewani siku maalumu na wanaizunguka televisheni au redio. Kwa mfano kipindi cha watoto wetu cha ITV hurushwa kila Jumamosi na tena Jumapili. Huu ni wakati watoto wanapopata fursa ya kuhadithiwa hadithi za fasihi simulizi, kuimbiwa nyimbo, kutegewa vitendawili, kufumbua mafumbo na kufafanua methali.

## 9.0 Uhifadhi na Uthabiti wa fasihi simulizi katika muktadha wa sayansi na teknolojia

Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, sasa fasihi simulizi inaweza kuhifadhika vizuri zaidi kuliko ilivyofikiriwa na wanamapokeo. Tena uthabiti wake ni wa kudumu, kwani leo hii simulizi yoyote inaweza kuwekwa katika mkanda kama wa kompyuta (flopy) au hata CD. Inaweza pia ikarekodiwa katika video na hata DVD na ikaendelea kuwapo kwa miaka mingi sawa sawa na fasihi andishi au hata zaidi. Kwa upande wa video na DVD, uhifadhi wake huendelea kuonyesha vitendo na sauti na huweza kudumu hata zaidi ya maandishi katika fasihi andishi kama itatunzwa vizuri. Hoja kwamba mtu akifa na fasihi simulizi inakufa, au kwamba sio thabiti inaweza kutofautiana kutoka mahali hadi mahali, zinakiuka suala la wakati na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Suala hili linaangaliwa kutoka katika hoja ya msingi kwamba, 'hulka ya fasihi simulizi imejengeka katika mwingiliano kati ya fanani, hadhira na muktadha'. Hoja hii ni mojawapo ya nguzo ninazoziita za kiuanamapokeo ambazo hazizingatii athari ziletwazo na mabadiliko katika sayansi na teknolojia kuhusiana na "hulka" ya fasihi simulizi. Kama nilivyoonyesha awali, wakati huu sio lazima kuwe na mwingiliano wa fanani, hadhira na muktadha; kama

kwa mwingiliano inamaanisha kuwa pamoja, kuonana ana kwa ana. Na kwahiyo, hulka ya fasihi simulizi kama ilivyokuwa hapo zamani, imebadilika kwa sasa. Fasihi simulizi haina budi kutazamwa kwa jicho la mabadiliko. Jicho ambalo halina budi pia kulitazama kipekee suala la "uhuru" wa msanii.

### 10.0 Uhuru wa msanii

Msanii wa fasihi simulizi hana uhuru sana kama akirekodiwa kwenye redio, video, DVD au televisheni au hata intaneti. Anapata uhuru tu wakati anapokuwa anaweza kuwasiliana na hadhira yake iwe katika vyombo hivyo au ana kwa ana, na anapokuwa na uhuru wa kubadili na kujifaragua.

Tumeona kwamba sifa nyingi au "hulka" za fasihi simulizi kwa mujibu wa wanamapokeo, zimebadilika au zimo katika mabadiliko. Nyingi kama sio zote, hazikutuama, bali zinasogezwa mbele na msukumo wa wakati na mahali. Ikiwa hivyo ndivyo, dhana ya fasihi simulizi iangaliwe zaidi kwa kuzingatia sauti, jambo ambalo makala haya yataligusia katika hitimisho.

### 11.0 Hitimisho

Fasihi simulizi ni sanaa inayosimuliwa, ambayo maana ya usanii wake umo katika sauti. Ikiwa usimuliaji utawekwa katika maandishi, basi jambo hilo litaiua dhana ya fasihi simulizi. Suala la sauti ndilo la msingi katika kuielewa dhana na maana ya fasihi simulizi, na wala sio tu chombo kama vile mdomo, au redio. Fafanuzi zilizotangulia zilikishadidia kipengele cha mdomo na kukipa umuhimu ambao hata hivyo unapungua kadri siku zinavyopita kutokana na mabadiliko hasa katika vipengele vya usambazwaji na uwasilishwaji. Kwa mfano, fafanuzi hizo ziliiona fasihi simulizi kama "aina ya fasihi ambayo hutumia mdomo katika kuumbwa, kuwasilishwa na kusambazwa kwa wasilikilizaji na watumiaji wake... (ambayo) hutegemea sana nyenzo mbalimbali za kuonekana na kusikika zitumiwazo na binadamu katika kujieleza." Maelezo haya yalikuwa ya kweli wakati fulani, lakini yanabadilika. Kutokana na ukweli huu wa maendeleo ya sayansi na teknolojia na athari zake kwa fasihi simulizi, mabadiliko katika usimuliaji yanaweza kuiathiri nadharia ya fasihi simulizi.

Kwa hakika dhana ya fasihi simulizi, na hali ya fasihi simulizi katika dunia inayoendelea haipaswi kuachwa iangaliwe kimapokeo, kama isiyobadilika. Hili suala ni sawa na yale mengine ambayo yanaakisi uhai wa jamii, halina budi kuangaliwa kulingana na maendeleo ya jamii, kisayansi na kiteknolojia. Hatuna budi kuwapa changamoto wasomaji na wasikilizaji wa fasihi simulizi ili waiangalie katika welewa huo na kujiuliza maswali ambayo yanaendana na wakati tuliomo na hata kuakisi wakati utakaokuja. Ingawa hili linahitaji utafiti wa kina, katika fasihi, sauti ina nguvu zaidi kuliko maandishi na athari zake za

kisanii zina mawanda mapana mno kuliko maandishi. Fasihi simulizi basi ina mashiko zaidi kisanaa kuliko fasihi andishi kama matawi haya ya fasihi yataangaliwa katika muktadha wa maendeleo ya sayansi na teknolojia.

## MAREJEO


Bal. M. 1997. Narratology: Introduction to the theory of Narrative 2nd Edition. Toronto: University of Toromto Press.

Balisidya, M.L. (Mrs. Matteru) 1979. *Utafiti, mbinu za ukusanyaji wa Fasihi simulizi na hatima yake.* Katika Lugha Yetu, Baraza la Kiswahili la Taifa Namba 34. Dar es Salaam:

Balisidya, M.L. 1980. *The image of the woman in Tanzania oral literature: A survey.* Katika Kiswahili Vol. 49, No. 2 Dar es Salaam: UDSM: TUKI.

Bukenya, A.S; Gachanja, M; Nandwa, J. 1997: Oral Literature: A senior Course. Nairobi: Longhorn Publishers.

Finnegan, R. 1970. Oral Literaure in Africa. Nairobi: Oxford University Press.

Kezilahabi, E. 1995. *Siasa, Teknolojia na ukuaji wa Fasihi ya Kiswahili* Katika Kioo cha Lugha , Juzuu 1, Dar es Salaam.

Matteru, M.L. B 1983. *Fasihi simulizi na Uandishi wa Kiswahili* katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III Fasihi. Dar es Salaam: UDSM: TUKI.

Mbunda, M. 1992. Kunga za Fasihi na Lugha., Dar es Salaam. Educational Publishers and Distributors Ltd

Mulokozi, M.M. 1989. *Tanzu za Fasihi Simulizi.* Katika Mulika, Na. 21 UDSM: TUKI. Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M. 1996 Fasihi ya Kiswahili OSW 105: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.

Okpewho, I. 1992. African Oral Literature: Background, Character, and Continuity. Bloomington: Indiana University Press.

Wamitila, K.W. 2003. Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi. Nairobi: Focus Publication.